



WorldVeg



# Kilimo cha Zao la Choroko Tanzania kwa Usalama wa Chakula, Lishe na Kipato Kwa Mkulima: Fursa, Changamoto na Suluhisho

P.H. Binagwa<sup>1</sup>, E.K. Mbeyagala<sup>2</sup>, J.W. Msaky<sup>1</sup>, F. Mmbando<sup>1</sup>, M. Makenge<sup>1</sup>, J.S. Joachimu<sup>1</sup>, E. Simfukwe<sup>4</sup>, R. Karimi<sup>3</sup>, R. M. Nair<sup>4</sup>

<sup>1</sup> Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania

<sup>2</sup> Shirika la Taifa la Utafiti wa Kilimo, Uganda

<sup>3</sup> Shirika la Taifa la Utafiti wa Kilimo na Mifugo, Kenya

<sup>4</sup> Kituo cha Kimataifa cha Utafiti wa Mboga mboga (World Vegetable Center)

\*Email: [hongera1984@yahoo.com](mailto:hongera1984@yahoo.com)



## UTANGULIZI

❖ Choroko ni zao la chakula na biashara lenye virutubisho vya protini na madini ya chuma na zinki kwa afya ya binadamu

❖ Hustawi katika udongo wa aina tofauti tofauti na usiotuamisha maji, hulimwa kutoka usawa wa bahari mita 0 mpaka 1500 na mavuno ni kati ya 1000-1500kg kwa hekali kulingana na ufuatiliaji wa Kanuni za kilimo bora cha choroko

❖ Tanzania tuna aina mbili za mbegu bora za choroko NURU na IMARA zilizopendekezwa mwaka 1982

❖ Uzalishaji wa choroko mwaka 2016/17 ni tani 73,073 kwa tija ya gunia 4 za kilo 100 kwa hektali moja

❖ Uzalishaji wa zaidi ya asilimia 78 unatoka mikoa ya Mtwara (27%), Simiyu (17%), Mwanza (14%), Tabora (12%) na Kilimanjaro (7%)

❖ Virutubisho vitokanavyo na choroko vinasaidia kupunguza udumavu na kuongeza afya kwa watumiaji

❖ Mradi huu unalenga kutafiti mbegu bora za choroko, kupunguza ukosefu wa Chakula na lishe, mabadiliko ya tabia nchi na uharibifu wa mazingira chini ya maendeleo endelevu ya umoja wa mataifa

❖ Hususani kupunguza utapiamlo miongoni mwa jamii katika maeneo yanayokabiliwa na ukame Afrika Mashariki.

## FURSA ZILIZOPO ZAO LA CHOROKO

➤ Choroko inaweza kulimwa katika aina zote za udongo na hali ya hewa, pia inaweza kuchanganywa na mazao mengine shambani na kurutubisha udongo

➤ Uwezo wa kuzalisha choroko mara mbili kwa mwaka kulingana na hali ya hewa nchini


➤ Tanzania inauwezo wa kuuza choroko kuanzia mwezi Februari hadi Mei bila ushindani ndani ya jumuiya ya Afrika Mashariki

➤ Uhusiano mzuri wa kiuchumi na India ambao ndio soko kuu la choroko kwa nchi za Africa

➤ Uwezo wa kuongeza uzalishaji kwa zaidi ya asilimia 50 kwa kufuata mbinu bora za kilimo cha choroko

➤ Uwezo wa virutubisho vya zinki, kalsium (chokaa) na chuma kwa wingi ambavyo ni muhimu katika ukuaji wa Watoto, afya ya uzazi na kuimarisha mifupa katika mwili wa binadamu.

Uzalishaji wa choroko kwa mikoa ya Tanzania 2016/17



Uzalishaji (Tani)



## CHANGAMOTO

- Uzalishaji usio na tija kwa mkulima
- Mabadiliko ya tabia nchi
- Ukinzani dhaifu wa magonjwa na wadudu
- Wadudu waharibifu wa ghalani
- Ukosefu wa upatikanaji wa mbegu bora za choroko
- Ukosefu wa upatikanaji wa pembejeo kwa wakati
- Ukosefu wa upatikanaji wa mbegu zenye tabia chanya kwa uzalishaji kama ukinzani wa magonjwa na wadudu waharibifu
- Gharama kubwa ya bei za mbegu zilizopo na upatikanaji hafifu
- Bei ya chini na isiyoridhisha kutoka kwa wanunuzi wa zao la choroko
- Ukosefu wa masoko ya uhakika ya choroko
- Miundombinu duni kwa baadhi ya maeneo yanayolima choroko.

## SULUHISHO

- Kutafiti mbegu bora za kilimo zenye ukinzani wa magonjwa na wadudu
- Kubuni teknolojia zitakazo ongeza tija kwenye mnyororo wa thamani wa zao la choroko
- Kuunganisha wakulima na masoko
- Kuhamasisha matumizi ya mbinu bora za kilimo cha choroko.

## FASIHI MUHIMU

1. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (2017). Ripoti ya Utafiti wa Kilimo Mwaka 2016/17 Ukurasa wa 46-48
2. Kilimo Trust (2017). Sifa za masoko ya zao la choroko ndani ya Jumuiya ya Africa Mashariki. Mradi wa kimataifa wa Jumuiya ya Africa Mashariki wa mazao muhimu ya mikunde.